# Global Schools Program




# Muhtasari wa Kozi

## Darasa la 2

---

**Chanzo:** Reimers, F. (2017). *Empowering students to improve the world in sixty lessons*. 1st ed. Createspace Independent Publishing Platform.

**Hati Miliki:** © 2017 Fernando M. Reimers. Kazi hii imeidhinishwa chini ya leseni ya kimataifa ya Creative Commons Attribution 4.0. Kutazama nakala ya leseni hii tembelea, https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/ Haki zote zimehifadhiwa.

**Taarifa:** Maudhui yote yaliyomo humu yameandaliwa  na kuchapishwa kwa kujitegemea na  Programu ya Shule za Kimataifa (Global Schools Program).

---

SUSTAINABLE DEVELOPMENT GOALS
17 GOALS TO TRANSFORM OUR WORLD

Global Schools Program

| Muhtasari | |
|---|---|
| **Lengo la kujifunza**<br>Kuhama kutoka kimataifa mpaka ndani ya nchi, wanafunzi watatambua sifa za jamii ya kimataifa, sifa za jamii yao mahalia, sifa za wanafunzi wenzao na sifa zao wenyewe. | |
| **Nguzo za Somo** | |
| **Somo la 1** | Kuudadisi Ulimwengu unaotuzunguka |
| **Somo la 2** | Kumuhoji mwanafunzi mwenzako |
| **Somo la 3** | Kumtambulisha mwanafunzi mwenzako |
| **Somo la 4** | Grafu upau za kirafiki |
| **Somo la 5** | Majadiliano na Tafakari |
| **Madhumuni ya Kujifunza** | |
| • Wanafunzi watatafiti na kugundua tofauti zilizopo darasani na ulimwenguni.<br>• Wanafunzi watajifunza zaidi juu ya nini kinachofanya wanafunzi wengine darasani kuwa wa pekee.<br>• Wanafunzi watakuwa wadadisi zaidi na kuvutiwa na tamaduni nyingine.<br>• Wanafunzi watafanya majaribio ya kuuliza maswali na kusikiliza kwa makini. | |

**Darasa la 2 Somo la 1**

"Kuudadisi Ulimwengu unaotuzunguka: Kuuliza Maswali yanayohusu Tamaduni, Mahali, na Uzoefu"

**Muda:** Dakika 30
**Mada:** Kusoma/Sanaa za Lugha
**Viwango:** Amani, Haki, na Taasisi Thabiti (SDG 16)
**Imebuniwa na:** Josie Papazis na Ben Searle

**Muhtasari na Mantiki:** Katika somo hili, walimu watatumia mwongozo wa maandishi na picha kuchochea shauku na jukwaa la udadisi wa wanafunzi. Kisha wanafunzi watafanya majaribio ya kuunda maswali sahihi ya kuwauliza wenzao kuhusu tamaduni zao, uzoefu wao na asili zao. Kwa kutumia vielelezo wanafunzi wanaweza kutambua maeneo ya udadisi na watatumia usaidizi wa mwalimu kuunda maswali sahihi na ya kiuchunguzi. Udadisi ni sehemu muhimu ya kujenga uelewa wa tamaduni pamoja na kuwafunza wanafunzi kuwa na utambuzi zaidi juu ya uelewa wa ulimwengu unaowazunguka.

**Lengo la Ufundishaji:** Wanafunzi wataweza ku...

- Elewa maana ya utofauti
- Tambua dhima ya utofauti katika maisha ya kila siku
- Tambua na kufurahia thamani ya utofauti

**Lengo la Uelewa:** Wanafunzi watajifunza namna ya kuunda maswali yaliyofikiriwa kwa kina, na kuhusu umuhimu wa kujifunza toka kwenye mitazamo ya wengine na uzoefu wa wengine.

**Maswali Muhimu:**

- Watu wengine wanafanana kwa namna gani na sisi?
- Wanatofautiana kwa namna gani na sisi?
- Ni kwa njia gani uzoefu wa watu unatengeneza maoni yao?
- Ni vitu gani tunaweza kujifunza toka kwa watu ambavyo hatuwezi kujifunza toka mahali pengine?

**Madhumuni ya Wanafunzi kujifunza:** Kwa kutumia vielelezo picha na udadisi wa kimtindo, wanafunzi wataweza kuuliza maswali yanayofaa, yenye msingi wa kidadisi kuhusu mapendeleo, maisha ya nyumbani, na desturi za kitamaduni.

**Tathmini:** Majibu ya wanafunzi katika mjadala wa kusoma na maswali kuhusu picha yanayoibuliwa na vikundi.

- **Mpangilio wa mazoezi:**
  - Mwalimu anasoma kitabu *Where Children Sleep* https://www.jamesmollison.com/where-children-sleep
  - Mwalimu anachagua watoto wa 3-4 kutoka katika kitabu na kuwauliza wanafunzi ni aina gani ya maswali wangewauliza watoto katika kitabu kama wangependa kuwafahamu vema.
  - Mwalimu anapaswa kuwaongoza wanafunzi kuelekea zaidi kwenye maswali ya wazi ambayo yatazalisha majibu kamilifu zaidi.
  - Mwalimu anaandika maswali ya mfano ubaoni.
  - Kisha mwalimu anaonesha darasa picha 4 za watu kutoka tamaduni tofauti, umri tofauti au makundi ya makabila tofauti; anauliza wanafunzi kama wanajua chochote au wangependa kujua chochote kuhusu watu walio kwenye picha.
  - Kwenye makundi ya wanafunzi watatu au wanne, tunga maswali matano kuhusu mtu mmoja kati ya watu waliopo kwenye hizo picha nne.

**Nyenzo kwaajili ya Waalimu:**

- *Where Children Sleep* na James Molleson: https://www.jamesmollison.com/where-children-sleep

**Darasa la 2 Somo la 2**

"Kumuhoji mwanafunzi mwenzako"

**Muda:** Dakika 45
**Mada:** Kiingereza/Sanaa za Lugha
**Viwango:** Amani, Haki na Taasisi Thabiti (SDG 16); Ubia ili kuyafikia malengo (SDG 17)
**Imebuniwa na:** Josie Papazis, Ben Searle, Vijayaragavan Prabakaran

**Muhtasari na Mantiki:** Kuendeleza ujuzi uliopatikana katika Somo la 1, wanafunzi watajijenga katika kuelewa hisia za wengine na kuongeza uelewa juu ya wenzao kupitia mfumo wa kuuliza maswali ya wazi na kusikiliza kwa makini. Wanafunzi watafuaatilia majibu ya wanafunzi wenzao kwa ajili ya kuwasilisha katika somo linalofuata.

**Lengo la ufundishaji:** Wanafunzi wataweza kuhoji wenzao, wakichukua maelezo kwa ajili ya kuwasilisha baadaye.

**Lengo la Uelewa:** Wanafunzi wataelewa kwamba wanapouliza maswali ya wazi yaliyofikiriwa kwa kina na kusikiliza kwa makini, wanaweza kujifunza toka kwa wenzao vitu ambavyo wasingeweza kuvifahamu kwa namna nyingine.

**Maswali Muhimu:**

- Ni nini ninajua tayari kuhusu mtu huyu?
- Ninataka kujua nini kuhusu mtu huyu?
- Kuna kilichonishangaza katika yale niliyojifunza kuhusu mtu huyu?
- Kuna kilichonisaidia kuwaelewa zaidi?
- Ninataka kujua nini sasa?
- Ni njia gani bora ya kuuliza maswali ili kupata taarifa hizo?

**Wanafunzi wataweza:**

- Kutunga maswali ya wazi kwa njia ya kuandika
- Kutambua upendeleo na asili za mwanafunzi mwingine kwa njia ya kusikia kwa makini

**Tathmini:** Mawasilisho ya wanafunzi.

**Mpangilio wa Mazoezi:**

★ **Sehemu ya 1:** Mwalimu anatoa maelekezo ya namna ya kutambua na kuunda maswali ya wazi. Maswali ya wazi yanaweza kutusaidia kugundua ni kipi kinafanya wengine kuwa wa pekee na tofauti. Hakuna jibu sahihi wala jibu lisilo sahihi kwa maswali ya wazi. Swali la wazi haliwezi kujibiwa kwa "Ndiyo" au "Hapana."

★ **Sehemu ya 2:** Kila Mwanafunzi ananakili mifano minne ya maswali ya wazi yaliyo hapo chini. Kisha kila mwanafunzi anatunga swali moja la wazi au maswali mawali mapya ya wazi ya kwake mwenyewe (Mfano: "Niambie kuhusu...?", "Ni nini...?", "Kwa namna gani...?", au "Kwa nini...?").

**Sampuli ya maswali kwaajili ya wanafunzi kutumia:**

- Niambie kuhusu kumbukumbu yako ya furaha kuliko zote.
- Nini maana ya kuwa "rafiki mwema?"
- Unafikaje shule asubuhi?
- Kwa nini unapenda shule?

★ **Sehemu ya 3:** Kufanya kazi katika jozi, wanafunzi watatumia orodha ya maswali kuwahoji wenzao ili kujifunza zaidi kuhusu wao. Wanafunzi watapokezana zamu za kuulizana maswali na kusikiliza kwa makini.

**Zoezi kwa wanafunzi:** Wanafunzi wanapaswa kuandika kile wanachojifunza kuhusu wenzao kwa kuandika maneno muhimu au kuchora picha ili kuwasaidia kukumbuka walichojifunza kuhusu wenzao.

★ **Sehemu ya 4:** Mwalimu ataongoza majadiliano ya tafakari kwa kutumia mwongozo huu wa maswali:

- Kuna yeyote anaweza kutushirikisha jambo jipya alilojifunza kuhusu mwenzake?
- Je, umegundua chochote ambacho unafanana na mwenzako?
- Ni kwa namna gani unafanana au kutofautiana na mwenzako?
- Ulijisikiaje mwenzako apokuuliza swali la wazi?
- Kama watu wote wangefanana, unadhani itapendeza? Kwa nini unadhani itapendeza au kwa nini unadhani haitapendeza?

**Darasa la 2 Somo la 3**

"Kumtambulisha mwanafunzi mwenzako"

**Muda:** Dakika 30
**Mada:** Sanaa ya Lugha
**Viwango:** Amani, Haki na Taasisi Thabiti (SDG 16); Ubia ili kuyafikia malengo (SDG 17)
**Imebuniwa na:** Josie Papazis, Ben Searle, Vijayaragavan Prabakaran

**Muhtasari na Mantiki:** Katika somo hili, wanafunzi watawasilisha matokeo ya mahojiano yao na wenzao. Kuweka mpangilio mzuri, walimu watawasilisha maswali elekezi kuongoza mawasilisho ya wanafunzi. Kwa kushirikisha matokeo ya mahojiano yao, wanafunzi watajenga ujamaa kati yao na kusaidia uelewa wa kiutamaduni.

**Lengo la ufundishaji:** Wanafunzi wataweza kuwasilisha matokeo ya mahojiano yao na wenzao kwa darasa lote.

**Lengo la uelewa:** Wote tunapouliza maswali ya kufikiri na kusikiliza kwa makini, tunaweza kufahamu vitu kuhusu darasa letu ambavyo tusingeweza kamwe kuvijua kwa njia nyingine na kujenga urafiki wenye maana zaidi.

**Maswali Muhimu:**

- Nimejifunza nini kwenye mahojiano yangu?
- Ni kwa namna gani nataka kuwasilisha nilichojifunza kwa wenzangu darasani?
- Nimejifunza nini kwenye mahojiano ya watu wengine?
- Ni kwa namna gani haya niliyojifunza yanaathiri jumuiya ya darasa letu na uhusiano wangu na wanafunzi wenzangu?

**Malengo ya wanafunzi kujifunza (Wanafunzi wataweza):**

- kukumbuka kikamilifu mahojiano yao kutoka kipindi kilichopita
- Kuwasilisha mambo mapya matatu mpaka matano waliyojifunza kuhusu wanafunzi wenzao

**Mpangilio wa mazoezi:**

★ **Sehemu ya 1:** Kwa kuongezea kwenye mazoezi yaliyopita, kila mwanafunzi atasimama na kushirikisha darasa mambo chanya machache waliyojifunza kuhusu wenzao. Wanafunzi watatumia maswali yafuatayo kama mwongozo:

- Wenzao ni kina nani?
- Wakoje?
- Kwanini wao ni wa pekee?
- Wanatofautiana na wewe kwa namna gani?
- Nini umependa kuhusu kumuhoji mwenzako?
- Je ulikuwa na wasiwasi kuuliza maswali? Kama jibu ni ndio, unahisi ni kwa nini ulikuwa na wasiwasi?

★ **Sehemu ya 2:** Kama nyongeza, wanafunzi wanaweza kutunga shairi, ngoma, mchoro, au kuleta zawadi ndogo ya kuwasilisha kwa wenzao ambayo ni kama kusherehekea au kuonyesha kitu wanachopenda kuhusu wenzao.

★ **Sehemu ya 3:** Mwalimu atawaongoza wanafunzi katika tafakari baada ya mawasilisho yote kufanywa kwa kutumia maswali elekezi yafuatayo:

- Je, kuna anayeweza kutushirikisha jinsi alivyojisikia wakati mwenzake aliposema jambo zuri kumuhusu?
- Je, kuna anayeweza kutushirikisha jinsi alivyojisikia alipokuwa anasema jambo zuri kuhusu mwenzake?
- Kwa nini unajisikia vizuri kusema mambo mazuri?
- Kwa nini unafikiri ni vizuri kuwa tofauti au wa kipekee?

**Grade 2 Lesson 4**
"Grafu Upau za Kirafiki"

**Muda:** Dakika 40
**Mada:** Sanaa ya Lugha, Hisabati
**Viwango:** Afya Bora na Ustawi (SDG 3); Amani, Haki na Taasisi Thabiti (SDG 16); Ubia ili kuyafikia malengo (SDG 17)
**Imebuniwa na:** Vijayaragavan Prabakaran

**Muhtasari na Mantiki:** Mwalimu atatoa kielelezo cha jinsi ya kukusanya na kuwakilisha taarifa katika grafu za upau ili wanafunzi waweze kuhesabu mitazamo tofauti katika darasa lao na kuelewa mambo yanayofanana ndani yao darasani.

**Lengo la kujifunza:** Wanafunzi watajifunza kuhusu njia mbalimbali za kuwasilisha taarifa kupitia kielelezo cha mwalimu.

**Lengo la Uelewa:** Jinsi ninavyowasilisha taarifa ina muhimu sawa na uhalisia wa taarifa yenyewe, na lazima nifikirie kwa makini kuhusu kile ninachotaka hadhira yangu ijifunze kutokana na mawasilisho yangu.

**Maswali Muhimu:**

- Kwa kawaida tunawasilisha vipi taarifa?
- Aina gani za uwasilishaji ni bora kwenye aina tofauti za taarifa?
  - Taarifa za Tarakimu na namba?
  - Mahojiano?
  - Maoni mengine?
- Ni kwa jinsi gani namna yangu ya kuwasilisha taarifa inaathiri namna watu watakavyoichukulia taarifa hiyo?

**Mpangilio wa Mazoezi:** Mwalimu anaongoza majadiliano ya wanafunzi kuhusu sifa za rafiki mzuri na kupanga taarifa katika grafu rahisi za upau.

**Mjadala uliopendekezwa:**
**Mwalimu:** "Ni neno gani moja ambalo ungetumia kumuelezea rafiki yako? Ni nini sifa za rafiki mzuri? Fikiria rafiki au mtu unayependa kutumia muda wako naye, na uandike maneno mawili au matatu yanayoelezea sifa zao."

Hiari: Mwalimu anaweza kuandika ubaoni orodha ya sifa za rafiki mzuri na wanafunzi wachague sifa toka kwenye orodha hiyo.

**Mwalimu:** "Wakati huu, ambapo kila mmoja wenu anaponiambia neno linalofafanua rafiki mzuri, nitaliandika."

*Anaandika ubaoni.*

**Mwalimu:** "Loo, tuna maneno mengi mazuri ubaoni, na baadhi yenu mnarudia maneno yale yale. Je! Haitakuwa vizuri kama sasa tutaziweka sifa za rafiki mzuri zilizotajwa zaidi kwenye grafu?"

*Mwalimu anazipanga taarifa katika makundi na, kuandika namba kwa kila sifa kulingana na ni wanafunzi wangapi walioorodhesha sifa hizo.*

**Mfano:** "Anafurahisha" – Wanafunzi 7, "Mwema" – Wanafunzi 5, "Anasaidia sana" – Wanafunzi 4, "Msafi" – wanafunzi 2

**Mwalimu:** "Ajabu! Sasa, tutajifunza jinsi ya Kuonesha sifa hizi kwenye picha ya upau."

*Mwalimu anachora grafu ya upau na kuwaambia wanafunzi kuwa makundi yatakuwa kwenye mstari na namba zitakuwa mstari wa wima.*

**Mwalimu:** "Hii inavutia sana! Sasa tunaweza kujua sifa muhimu zaidi za rafiki mzuri kwa kuangalia tu picha hii. Hii pia inaitwa grafu ya upau."

*Mwalimu anaangalia uelewa.*

**Mwalimu:** "Sasa, tutatengeneza grafu nyingine ya upau, lakini mara hii tutafanya kwa pamoja."

*Mwalimu atachagua mwanafunzi na kumuuliza swali ambalo angependa kujua kuhusu darasa zima (mfano "Rangi//mnyama/chakula gani unachopenda zaidi?"). Mwalimu atamsaidia mwanafunzi kukusanya taarifa na kuziandika kwa njia ya nambari, na kisha kuzichora taarifa hizo kama grafu ya upau.*

**Mazoezi binafsi ya hiari:**

- Katika makundi wanafunzi wanatumia taarifa ambazo tayari wamekusanya kutoka kwa masomo ya awali kuhusu marafiki zao, na kuwasilisha taarifa hizo katika grafu.
- Katika makundi wanafunzi wanafanya mradi/projekti nje ya darasa kuhusu maswali ambayo yanaweza kuweka msingi wa umahiri wa Mpango wa Malengo endelevu (SDGs):
    - Ni mara ngapi umesaidia wengine wiki hii?
    - Marafiki zako wangapi wanazungumza lugha tofauti?
    - Ni mara ngapi umeshirikisha wengine kitu?

**Darasa la 2 Somo la 5**

"Majadiliano na Tafakari"

**Muda:** Dakika 20
**Mada:** Sanaa ya Lugha, Hisabati
**Viwango:** Amani, Haki na Taasisi Thabiti (SDG 16); Ubia ili kufikia malengo (SDG 17)
**Imebuniwa na:** Josie Papazis, Ben Searle

**Muhtasari na Mantiki:** Ni muhimu kuhakikisha kwamba wanafunzi wanatambua umuhimu wa kuuliza maswali na kwa nini tunatumia maswali kujenga kufahamiana. Kupitia tafakari yenye muongozo, wanafunzi watafakari juu ya mafunzo na kujadili jinsi ya kuhamisha ujuzi huu kwa muktadha wa nje ya darasa ili kuuliza maswali yahusuyo wenzao na ulimwengu unaowazunguka.

**Lengo la kujifunza:**
Wanafunzi wataweza kuzingatia walichojifunza kuhusu kuuliza maswali makini, na kutafakari jinsi wanavyoweza kuleta mafunzo haya katika maisha yao ya kila siku.

**Lengo la uelewa:** Ujuzi niliojifunza kwa kuwahoji wanafunzi wenzangu pia unaweza tumika kwenye mahusiano yangu na watu wengine nje ya darasa, na ninapaswa kuendelea kuuliza maswali ya kufikiria na kusikiliza kwa makini katika maisha yangu.

**Maswali Muhimu:**
- Nimejifunza nini kuhusu kuuliza maswali na kutafsiri majibu katika darasa hili?
- Kuna chochote kilichonishangaza, au sikuwahi kukifikiria kabla?
- Kuna mazingira au maeneo mengine ambapo ujuzi na masomo haya yatakuwa na faida? Kama jibu ni ndio, ni maeneo yapi?

**Malengo ya mwanafunzi kujifunza (Wanafunzi wataweza):**
- Kutafakari juu ya mahojiano na mchakato wa kuuliza maswali
- Kushirikisha mawazo na tafakari zao kwa darasa lote

**Mpangilio wa Mazoezi:** Mwalimu ataongoza darasa katika maswali yafuatayo...
- Ni kipi kilikuwa kigumu kuhusiana na mazoezi haya?
- Je ilikuwa rahisi kuzungumza na mwenzako?
- Ni kitu gani umejifunza kuhusu mwenzako ambacho hukukijua kabla?

**Mada na Matokeo Lengwa:**
- Kukubali tofauti/ kuvumiliana
- Kujifunza kwa kushirikiana